

# **MKOA WA DAR ES SALAAM**

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UCHAGUZI WA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2018 KATIKA MKOA WA DAR ES SALAAM**

Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na jumla ya wanafunzi **66,978** waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka huu 2017. Kati yao wavulana ni **31,911** na wasichana **35067**. Idadi ya watahiniwa waliofanya mtihani huo ni **66,695** sawa na asilimia **99.58**, kati yao wavulana ni **31,760** na wasichana ni **34,935**. Watahiniwa **283** sawa na asilimia **0.42** hawakufanya mtihani huo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo utoro wanafunzi **241**, vifo **15**, ugonjwa **17** na sababu zingine **10**. Idadi ya wasiofanya imeshuka kutoka wanafunzi **715** mwaka 2016 hadi wanafunzi **283** mwaka 2017.

Watahiniwa **58,573** (Wavulana **28,103** na wasichana **30,470**) sawa na asilimia **87.82** wamefaulu mtihani huo. Ufaulu huo umepanda kutoka asilimia **82.58** ya mwaka 2016 hadi asilimia **87.82** kwa mwaka 2017 sawa na asilimia **5.24**. Matokeo hayo yameufanya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa katika nafasi ya kwanza (**01**) Kitaifa. Aidha, wanafunzi wote **58,573** waliofaulu sawa na **100%** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari, 2018 hivyo kwa mwaka huu hatutakuwa na chaguo la pili.

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule za ufaulu mzuri zaidi ni **68** wavulana **35** na wasichana **33**. Shule za Ufundi **74** wavulana ni **68** na wasichana **6**. Shule za Bweni kawaida **24**, wavulana **12** na wasichana **12**. Katika Shule za Mkoa zinazochukua wanafunzi wa Mkoa wa Dar es Salaam jumla ya wanafunzi **1,931** wamechaguliwa, ambapo wavulana ni **850** na wasichana **1,081**. Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga katika Shule za Sekondari za Serikali za Wananchi ni **56,299** ikiwemo wavulana **27,035** na wasichana **29,264**. Wanafunzi wenye mahitaji maalum waliopangwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI **101** wavulana ni **58** na wasichana **43**.

Kwa ujumla waliochaguliwa kwa Manispaa ya Ilala ni **19,236**, Kigamboni **2,803**, Kinondoni **10,885**, Temeke **15,323** na Ubungo ni **10,326**.

Zipo nafasi **4,685** katika shule za pembezoni/vijijini ambazo zimebaki wazi kwa sababu ya umbali uliopo kati ya Shule ya Msingi waliposoma wanafunzi na mahali Shule hizo zilipo (catchment area). Nafasi zilizobaki kwa Manispaa ya Ilala ni **887**, Kigamboni **590**, Kinondoni **1,718** na Ubungo **1,490**.

Kuhusu asilimia ya wanafunzi ya kujiunga na Shule za Sekondari kwa waliofanya mtihani (transition rate) kwa Mkoa ni asilimia **87.82**. Katika Manispaa ya Ilala (Mjini) ni asilimia **92,48**, Ilala (Vijijini) asilimia **84.42**, Kinondoni asilimia **93.02**, Temeke asilimia **81.74**, Kigamboni **91.10** na Ubungo **89.01**. **Hivyo idadi kubwa zaidi ya wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba wamepata nafasi za kujiunga na Shule za Sekondari Manispaa ya Kinondoni ikifuatiwa na Ilala Mjini, Kigamboni, Ubungo, Ilala Vijijini na Temeke.**

Kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa jitihada inazozifanya kuhakikisha Mpango wa upatikanaji wa Elimu msingi bila Malipo unatekelezwa kama uliovyokusudiwa. Nawashukuru pia Maafisa Elimu, Walimu, Wadau wa Kamati za Shule katika Manispaa zote kwa juhudi za usimamizi na uboreshaji wa utoaji wa elimu mzuri, pamoja na wazazi na walezi wote kwa malezi na ufuatiliaji wa watoto wao.

Nachukua fursa hii kuwataka wazazi na walezi wa wanafunzi hawa kuwapeleka watoto wao kwenye shule walizopangiwa tarehe **8/01/2018** bila kukosa. Aidha, ninawakumbusha Wakuu wa Shule **147** zinazopokea wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kuzingatia **Waraka wa Elimu Namba 2 wa mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa Elimumsingi bila Malipo.**

Nazishukuru Kamati za Uendeshaji wa Mitihani za Wilaya na Mkoa, Sekretarieti ya Uchaguzi wa Wanafunzi ya Mkoa kwa kufanya kazi hii kwa umakini na uadilifu mkubwa, lakini pia Kamati ya Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza ya Mkoa kwa kukamilisha kazi hii muhimu na kwa ufanisi. Orodha ya Majina ya wanafunzi waliochaguliwa inapatikana kwa kila Mratibu Elimu Kata, Mbao za Matangazo za kila Halmashauri na Website ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo ni [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz).

**Theresia Mmbando**  
**KATIBU TAWALA WA MKOA**  
**DAR ES SALAAM**